# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA
# NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA.

SHULE YA SEKONDARI LIKUNJA,
S.L.P. 140.
**RUANGWA.**
TAREHE………………

***Kumb. Na. LKS 3905/UI/14***

Jina la Mwanafunzi………………………………
S.L.P. 51
……………………………………..

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI LIKUNJA MWAKA 2021.</u>**

Husika na kichwa cha habari hapo juu. Ninayofuraha kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Likunja mwaka 2021.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo unatakiwa kuziosoma kwa makini na kuzifanyioa kazi.

i. Fomu ya mahitaji muhimu ya shule.
ii. Fomu ya kupimwa afya ya mwanafunzi kutoka kwenye Hospitali inayotambulika na serikali
iii. Fomu ya sheria za shule.
iv. Mkataba wa mwanafunzi wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021, hivyo kamilisha mahitaji mapema na kuwahi shuleni. Unatakiwa kuripoti shuleni kabla ya tarehe 18/01/2021.

**NB:** Unapokuja kuripoti fika na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.
Mwisho nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa shuleni.
Karibu sana Shule ya Sekondari Likunja.

**EDUCATION FOR POVERTY ALLEVIATION**

**……………………………….**
**GRACE E. MALLYA**
**MKUU WA SHULE.**
**Simu Na. 0715 130321**

# MAHITAJI MUHIMU YA SHULE.

1. **Sare ya Shule.**
   a) Suruali mbili (02) za rangi ya kijivu kwa wavulana ziwe zimeshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo (zisishonwe modo) upana uwe sm 17.
   b) Sketi mbili (02) za rangi ya kijivu kwa wasichana ziwe zimeshonwa kwa unadhifu bila madoido au mitindo, sketi ndefu kupita magoti na rinda box. Kwa wanaovaa hijabu sketi ifike chini.
   c) Mashati meupe mawili kwa wavulana na wasichana ya mikono mifupi yenye kola shingoni nusu kanzu na ijabu ndefu kama ni mwiislamu.
   d) Viatu vya ngozi jozi mbili (02) viatu visiwe na urembo wowote wala visiwe vya kupanda au visigino virefu.
   e) Soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
   f) Tranki suti nyeusi na raba kwa ajili ya michezo.

2. **Mahitajhi kwa ajili ya taaluma.**
   a) Daftari za kutosha kaunta book kumi na mbili (12) na zaidi)
   b) Kalamu za wino za bluu au nyeusi za kutosha.
   c) Kalamu za Risasi (penseli)
   d) Mathematical Set, Rula ndefu futi 1.
   e) Kamusi (Dictionary) ya Kiingereza na Kiswahili.
   f) Rimu 1 A4 nyeupe.

**NB: Kitambaa cha sare kinapatika dukani kwa Mama Komba Likunja stendi.**

3. **Vifaa vya usafi**
   a) Ndoo kubwa 1
   b) Jembe lenye mpini
   c) Panga/slesha
   d) Reki
   e) Fagio (softbloom).

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA.

**SHULE YA SEKONDARI LIKUNJA, S.L.P. 140 – RUANGWA – LINDI.**

**Ref. No……………………………………**

**To Medical Officer**

…………………………………………………
…………………………………………………
…………………………………………………

**RE. REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF …………………………………………**

Please examine the above named pupil/student and give us a report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

Pupils full name……………………………………………………………………….………

1. Blood ……………………………………………………………..………………
2. Stool …………………………………………………………………………………….
3. TB test………………………………………………………………………….………
4. Syphilis test …………………………………………..…………………………
5. Urine examination ……………………………………………………………………
6. Eye test ……………………………………………………………………………
7. Ear test ……………………………………………………………………………
8. Chest test …………………………………………………………………………
9. Spleen test …………………………………………………………………………
10. Abdomen……………………………………………………………………………
11. Pregnancy test (for girls) ……………………………..………………………………

Any other additional information; eg. Physical defects or impairment, infection, family disease.etc…………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

I declare that information given above is true and I certify that the named student is suitable/ unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**Name of the medical officer ………………………………………..signature………………..**

**Date ……………………………………………………..official stamp ………………………..**

**Fomu NA. 04(b)**

# SEHEMU B: HABARI ZA MLEZI/ MZAZI

Jina kamili ……………………………………………………

Kazi ……….……………………………………………

Nyumbani ……………………………………………………

Kata ……………………Mkoa ……………………..…

Tarafa ……………………Wilaya………………………

(a) Anuani ya mahali/makazi…………………………………………………

……………………………………………………………………….

……………………………………………………………………….

(b) Nambari ya simu ……………………………………………………

Dini ……………………………………Dhehebu…………………………

Anuani kamili ya nyumba ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo.

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

Ninaahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya kusoma.

Mimi ……………………………………………………mzazi/mlezi ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi.

Tarehe …………………………………sahihi………………………….

# MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi ……………………………………………………………………… nimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule, kwa hiari yangu nakubaliana nayo. Naahidi nitaheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Aidha naahidi kuwa, kwa vyovyote vile sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sheria, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo, fujo na kutenda makosa ya jinai. Basi nichukuliwe hatua stahiki kulingana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya Mwanafunzi na tarehe ……………………………

Saini ya Mzazi/Mlezi na tarehe ……………………………

Saini ya Mkuu wa shule na muhuri ……………………………

Tarehe ……………………………

**TAMKO LA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI ZA SHULE PAMOJA NA KUTEKELEZA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA.**

Mimi ……………………………………………

Mzazi/mlezi wa …………………………………………….

Nimeyasoma kwa makini maelekezo yaliyopo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya Sekondari Likunja.

Kwa hiari yangu, nakubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kuwa nitamsisitiza kuheshimu na kufuata taratibu, kanuni na sheria za shule.

Endapo mwanangu atavunja sheria, kanuni na taratibu za shule basi achukuliwe hatua stahiki kulingana na kosa atakalolifanya.

Aidha naahidi kuwa nitatekeleza malekezo yatakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini au shule.

Pia naahidi kusimamia taaluma, nidhamu, tabia na mwenendo wa mtoto wangu kwa kushirikiana na walimu naungozi wa shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi na tarehe ….………………………………

Saini ya Mwanafunzi na tarehe ………………………………

Saini ya Mkuu wa shule na muhuri ………………………………

Tarehe ……… ………………………

# SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha unatakiwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kuhudhuria katika shughuli zote ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
c) Kushiriki kwa makini katika masomo.
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Ni kosa kwa mwanafunzi kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote wa shule na unapokwenda nje kwa shughuli ya shule.
h) Kuzingatia ratiba ya shule na kutunza mali ya Umma.

**Makosa yafuatayo yanaweza yakasababisha ukafukuzwa shule.**

a) Wizi.
b) Uasherati na Ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.,
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuoa au kuolewa.
i) Kupata mimba au kuharibu mmba ndani na nje ya shule.
j) Kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
k) Kugoma, kuchochea nakuongoza au kuvuruga Amani na Usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

**(NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU)**